



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَاتُوا مِنْكُمْ وَعَجِلُوا إِلَيْنَا لِيَسْتَغْفِرُوكُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَغْفِرُ
الَّذِينَ مِنْ قَلْبِهِمْ وَإِنْ يَكُنْ لَّهُمْ أَثْقَلُ الْأَرْضِ فَمُمْكِنٌ لَّهُمْ وَلَكُبُولُهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْفِهِمْ أَنْتَ
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Taarifa kwa Vyombo vyta Habari

Madai ya Tovuti ya France 24 ni ya Uongo na ya Kashfa katika Jaribio la Mbaya la Kuficha Harakati ya Amani katika eneo la Kaskazini lililo Kombolewa (Imetafsiriwa)

Katika ripoti ya kushangaza ya vyombo vyta habari juu ya ukamataji na maandamano ambayo yamefanyika katika maeneo yaliyokombolewa kwa zaidi ya miezi miwili, waangalizi wa France 24 walitushangaza kwa mkusanyiko wa uwongo wa makusudi ambao chaneli kama France 24 haifai kufanya isipokuwa ikiwa wahariri wake bado wangali chini ya athari ya mshtuko wa maandamano yaliyozuka katika nchi yao iliyokumbwa na mgogoro. Endapo tutapuuza makosa ya kimbinu katika kuandaa ripoti, kama vile kutaja vijiji na miji ilioiasi kwa majina tofauti, kama walivyoita Al-A'tma badala ya Atmeh, Deir Al-Hasan badala ya Deir Hassan, Al-Sharara badala ya Al-Sahara, Al-Sarmada badala ya Sarmadah, na Hamas badala ya Hama, pia ilitajwa kuwa tume inadhibiti maeneo ya Al-Hasakah, ambayo ni jirani na Aleppo na Hama, na taarifa zote mbili sio sahihi. Tunasema: Ikiwa tulipuuza makosa haya ya kimbinu na tukasimama kutaja uongo mkubwa katika ripoti hiyo, ambapo hadithi ya kubuni imesukwa kuhusu matukio. Ambapo ripoti hiyo iliifafanua Hizb ut Tahrir kama "kundi la ndani la Kiislamu lenye wapiganaji... Hizb haikuwa chini ya uhangaishaji, lakini tangu Februari mwaka jana ilianza kubeba silaha... Baada ya wapiganaji wake kufyatulia risasi gari la usalama na kumuua mmoja wa wanachama wake, msako ulianza!" Tukizungumzia hadithi hii ya uongo, tunasema:

Kwa kuanzia, Hizb ut Tahrir sio kundi la kijeshi la ndani, na haina wapiganaji, kama ripoti ilivyotaja. Badala yake, ni chama cha kisiasa cha kimataifa, na hakina mrengo wenye silaha. Wanachama wake hawakubeba silaha Februari iliyopita, au Februari nyingine yoyote! Zaidi ya hayo, wanachama wa Hizb hawakuhangaishwa na kukamatwa na Hay'at Tahrir al-Sham katika miezi hii miwili pekee, kama ulivyotaja, bali kwa miaka iliyopita, tangu wakati viongozi wa Hay'at Tahrir al-Sham. (HTS) walipoamua kufuata mradi wa Magharibi unaolenga kuyamaliza mapinduzi. Ama kuhusu kampeni hii ya ukamataji, haikuza baada ya tukio la mauaji lilitotajwa kwenye ripoti, bali kabla yake. Na kisa kilichotajwa kwenye ripoti kuhusu mauaji hayo ni kisa kile kile cha mtu asijejulikana aliyejifunika uso wake, Diaa al-Omar. Ama kuhusu ukweli, mnaweza kuupata kwa kwenda tu mitaani katika vijiji hivi vya waasi na kumuuliza mtakayemkuta huko, sio kwa kukariri kama kasuku yale waliyoyasimuliwa waongo kwenye vyombo vyao rasmi vya habari!

Hatimaye, tunasema kwamba mkitaka kuandika ripoti nyingine za vyombo vyta habari kuhusu suala hilo, mnaweza kuusifia uhalisia jinsi ulivyo bila kudanganya na kupotosha ukweli. Vyenginevyo, ni bora kwenu kuwaacha watu waliokoloniwa kutokana na maovu yenu, na mijishughulishe na migogoro ambayo Ufaransa ya kikoloni inateseka nayo.

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Syria